- Maneno yaliyotamkwa au kitendo kilichofanywa si kosa la jinai na ni halali kisheria.
- Kama kosa la jinai lililofanywa linatokana na ushawishi, kusisimka na jazba ambazo zimetokana na mtu mwingine au matendo ya mtu mwingine.
- Kitendo halali kinachofanywa na vyombo vya dola katika kukamata watuhumiwa, isipokuwa kama itathibitika kwamba kitendo hicho hakikuwa halali na ni kinyume cha sheria.

### 2.1.9 Kuadhibiwa kwa Kosa Hilohilo

Mtuhumiwa aliyewahi kuadhibiwa kwa kosa hilohilo ana utetezi kwa sababu ni kanuni ya sheria kuwa mtu hataadhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile.

### 2.1.10 Kushitakiwa na Kuachiwa Huru

Hali kadhalika, mtu hatashitakiwa kwa kosa ambalo alikwisha shtakiwa na kuachiwa huru kwa kutopatikana na hatia au kwa sababu nyingine ya msingi itakayotolewa na upande wa mashitaka.

## HITIMISHO

Utetezi katika makosa jinai ni hatua muhimu katika mfumo wa haki jinai. Lengo kubwa ni kutoa nafasi kwa mshitakiwa kujitetea katika mashtaka yake. Utetezi unaipa mahakama nafasi ya kusikiliza pande zote katika shauri husika na kuhakikisha haki inatendeka kwa pande zote na hivyo mshitakiwa atakayetiwa hatia kupata adhabu stahiki baada ya kusikilizwa.

**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**


Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA




# UTETEZI KATIKA MAKOSA YA JINAI

## UTETEZI KATIKA MAKOSA YA JINAI

### 1.1 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa. Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu katika maboresho ya sheria.

### 2.1 HAKI YA KUSIKILIZWA

Haki ya kusikilizwa kabla ya kutiwa hatiani ni haki ya asili inayojumuisha mtu kufahamishwa shitaka linalomkabili kikamilifu; pamoja na kupatiwa muda wa kuandaa utetezi katika kujibu shtaka hilo. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaainisha haki ya kusikilizwa na Kanuni ya Adhabu ndio sheria mahususi inayoainisha aina mbalimbali za utetezi katika makosa ya jinai. Katika makosa ya jinai, Jamhuri inamshtaki mtuhumiwa na kutoa ushahidi ili kuthibitisha tuhuma dhidi ya mshtakiwa. Mshitakiwa pia ana haki ya kutoa ushahidi wake ili kujitetea dhidi ya tuhuma anazokabiliwa nazo.

#### 2.1 .1 Aina za Utetezi Katika Makosa ya Jinai

Mshtakiwa anaweza kuwa ametenda kosa la jinai lakini kitendo hicho cha jinai kinaweza kuwa kimetokana na sababu ambazo kisheria zinaweza kuwa ni utetezi wa kosa hilo.

#### 2.1.2 Ugonjwa wa Akili

Mtu anapokabiliwa na shtaka la jinai, anaweza kuwasilisha utetezi wa ugonjwa wa akili mbele ya mahakama. Hata hivyo mshtakiwa anatakiwa kuthibitisha kwamba wakati anatenda kosa hilo alikuwa katika hali ya ugonjwa ambao uliathiri akili yake kiasi

- Hakuweza kujuwa anachotenda au
- Hakuweza kujuwa kuwa hapaswi kutenda alichotenda.

#### 2.1.3 Msukumo wa Ulevi

Hali ya ulevi inaweza kuwa utetezi katika kosa la jinai endapo itathibitishwa kuwa wakati anatenda kosa, mtuhumiwa alikuwa amelewa kwa kiwango cha kutotambua anafanya kosa. Utetezi huu utakubalika tu pale itakapothibitika kuwa mtuhumiwa ameleweshwa na mtu mwingine kwa hila na ulaghai bila ridhaa yake; na kuwa akili ya mtuhumiwa iliathirika kwa ulevi kiasi cha kutojitambua wakati anatenda kosa.

#### 2.1.4 Umri Mdogo Chini ya Miaka Kumi

Mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi (10) hawajibiki kijinai kwa kutenda kosa la jinai. Vilevile mtoto mwenye umri wa chini ya miaka kumi na mbili (12) hawajibiki na kosa lolote la jinai, isipokuwa kama itathibitishwa kuwa wakati wa kutenda jambo hilo, alikuwa na uwezo wa kujua kuwa hapaswi kutenda au kuacha kutenda jambo hilo. Mtoto wa kiume mwenye umri wa chini ya miaka kumi na mbili (12) pia anachukuliwa kuwa hawezi kufanya tendo la ndoa.

#### 2.1.5 Kujilinda au Kujihami

Matumizi ya nguvu ya kujihami au kujilinda ni utetezi katika kosa la jinai. Kanuni ya Adhabu inatoa haki ya kujilinda binafsi au kumlinda mtu mwingine dhidi ya kitendo chochote kilicho kinyume na sheria ikiwemo shambulio au utumiaji nguvu dhidi ya mwili; kulinda mali binafsi au mali yoyote iliyo chini ya umiliki, himaya au chini ya uangalizi wake au mali ya mtu mwingine yeyote dhidi ya kuchukuliwa isivyo halali, kuharibiwa au kufanyiwa fujo. Hata hivyo, matumizi ya nguvu yanapimwa dhidi ya kitisho kilichopo. Kwa hiyo nguvu itakayotumika na mshtakiwa ni lazima iwe na uwiano na madhara yaliyotegemewa kutokea kwake.

#### 2.1.6 Kushurutishwa Kutenda Kosa la Jinai

Mshtakiwa anaweza kujitetea kuwa alilazimishwa au kushurutishwa kutenda kosa kwa kutishiwa kuuwawa au kuumizwa. Hata hivyo vitisho vya kuumizwa hapo baadaye havichukuliwi kuwa utetezi wa kosa lolote. Mfano mshtakiwa analazimishwa kujeruhi au kuua mtu na asipofanywa hivyo anapigwa risasi huku anayetoa amri akiwa amemwelekezea bastola mshitakiwa.

#### 2.1.7 Kutokuwepo Eneo la Tukio

Mshtakiwa atakuwa na utetezi endapo atathibitisha kuwa wakati kosa la jinai analoshtakiwa nalo likitendeka, hakuwepo eneo la tukio mfano anaweza kuwa alikuwa safari au amelazwa hospitalini n.k. Hata hivyo, mshtakiwa anatakiwa kuthibitisha utetezi wake huo kwa mfano anaweza: kuita mashahidi; kuwasilisha picha za cctv, risiti, tiketi au vyeti husika vya uthibitisho. Hata hivyo mshtakiwa anatakiwa kutoa taarifa kuwa atatoa wa utetezi wa kutokuwepo eneo la tukio.

#### 2.1.8 Kukasirishwa

Pale ambapo mtu anatenda kosa la jinai linalosababisha kifo akiwa katika hali ya joto la hasira kali iliyopandishwa ghafla na maneno au kitendo cha maudhi ambacho akitendewa mtu wa kawaida au kikitendwa mbele ya mtu wa kawaida kwa mtu mwingine aliye chini ya uangalizi wake kwa mfano: mke, mume, mzazi, mtoto wake, ndugu, tajiri au mtumishi, kina uwezo wa kumpandisha hasira na hivyo kushindwa kujizuwia nafsi yake na kufanya shambulio lililosababisha kosa la jinai.

Kitendo hiki cha mauaji ambacho mshtakiwa angewajibika kwa kosa la kuua kwa kukusudia, kinatakiwa kiwe kimefanyika kwa ghafla kabla ya hasira kupoa. Mazingira haya ya kusababishiwa hasira kali ya ghafla hutoa utetezi wa kukasirishwa na kupunguza hatia kuwa ya kuuwa bila kukusudia. Maneno au matendo ya kashfa ni lazima yatimize kigezo cha kumwondolea mtu wa kawaida uwezo wa kujizuia na kumshurutisha bila kupenda, kutenda kosa la jinai la shambulio dhidi ya mtu anayetoa au kufanya hayo matendo. Hata hivyo kukasirishwa sio kinga katika utetezi iwapo: